

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO



MKUTANO WA SABA

KIKAO CHA HAMSINI NA TATU

28 JUNI, 2022



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA SABA

KIKAO CHA HAMSINI NA TATU – TAREHE 28 JUNI, 2022

I. DUA:

II. MASWALI:

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

464. MHESHIMIWA OLIVER DANIEL
SEMUGURUKA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Serikali itajenga kingo za Mto Kanoni unaopita katikati ya Mji wa Bukoba.

WIZARA YA AFYA:

465. MHESHIMIWA ABDALLAH DADI CHIKOTA
(NANYAMBA):


Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:-

Je, ni lini Serikali itapeleka Watumishi wa kutosha katika Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Kusini iliyopo Mtwara.

466. MHESHIMIWA JESCA JONATHANI MSAMBATAVANGU (IRINGA MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:-

Je, ni lini ombi la kubadilishana Hospitali ya Mkoa na ya Wilaya litafanyiwa kazi kuruhusu upanuzi wa Hospitali ya Mkoa wa Iringa.



WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:

467. MHESHIMIWA AIDA JOSEPH KHENANI (NKASI KASKAZINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kupitia upya mipaka ya Hifadhi na Makazi ya Wananchi Wilayani Nkasi.


**468. MHESHIMIWA DANIEL BARAN SILLO
(BABATI VIJIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-

Je, ni lini Serikali itamaliza migogoro ya mipaka kati ya Vijiji vya Vilima Vitatu, Mwada na Ngolee dhidi ya Hifadhi ya Tarangire.

WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO:

**469. MHESHIMIWA JUMA USONGE HAMAD
(CHAANI):**



Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:-

Je, kuna mpango gani wa kupunguza Kodi, Tozo na Ushuru wa bidhaa za chakula/mboga kutoka Tanzania Bara kwenda Zanzibar.

**470. MHESHIMIWA LUHAGA JOELSON MPINA
(KISESA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:-


Je, kwa kiwango gani Serikali inakagua miamala ya uhamishaji wa bei ya mauziano ya bidhaa/huduma ya Kampuni za Kimataifa.

WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

471. MHESHIMIWA JULIANA DANIEL SHONZA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, ni lini ujenzi wa Kituo cha Polisi cha Mji Mdogo wa Mlowo utaanza baada ya kilichopo kuwekewa alama ya kubomolewa.



WIZARA YA MAJI:

472. MHESHIMIWA DKT. JASSON SAMSON RWEIKIZA (BUKOKA VIJIJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, ni lini ujenzi wa mradi wa maji Kemondo – Maruku katika Jimbo la Bukoba Vijijini utakamilika.

**473. MHESHIMIWA EMMANUEL PETER
CHEREHANI (USHETU):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka maji ya Ziwa Victoria katika Halmashauri ya Ushetu.

III. MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI:

***(Kusomwa Mara ya Pili, Kamati ya Bunge Zima
na Kusomwa Mara ya Tatu)***



Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2022 (*The Finance Bill, 2022*).

(Majadiliano yanaendelea)

**DODOMA
28 JUNI, 2022**

**N.J. MWIHAMBI, *ndc*
KATIBU WA BUNGE**